# MPANGO SHIRIKISHI WA USIMAMIZI NA UTUNZAJI

# MSITU WA

# HIFADHI WA MILAWILILA

**Umetayarishwa na**
**Kamati za Mazingira za vijiji vya Milawilila na Mifulu**
**July 2006**

# YALIYOMO

Yaliyomo……………………………………………………………………………………..i

Orodha ya Majedwali………………………………………………………………………ii

Orodha ya Michoro…………………………………………………………………………ii

Orodha ya Viambatanisho…………………………………………………………….....ii

Orodha ya Vifupisho na Kirefu Chake…………………………………………………...ii

Utangulizi……………………………………………………………………………………1

Maelezo Kuhusu Msitu ……………………………………………………………………1

Malengo ya Mpango Shirikishi ……………………………………………………..……6

Mfumo wa Usimamizi wa Msitu …………………………………………………………8

Mfumo wa Kutoa Taarifa…………………………………………………………………...12

Kanuni na Taratibu…………………………………………………………………………13

Namna ya Kuwashughulikia Wahalifu……………………………………………………14

Mapato na Matumizi yatokanayo na Faini………………………………………………..16

Ufuatiliaji………………………………………………………………………………………..17

Viambatanisho…………………………………………………………………………………19

## ORODHA YA MAJEDWALI

**Jedwali** **Ukurasa**

1 Takwimu muhimu za vijiji vinavyouzunguka msitu wa Milawilila…………………...5

2 Huduma zitolewazo katika Msitu wa Milawilila na kiasi cha malipo……………...13

## ORODHA YA MICHORO

**Mchoro** **Ukurasa**

1 Msitu wa Hifadhi wa Milawilila……………………………………………………….2

2 Ramani ya Milima ya Uluguru ikionyesha eneo msitu wa Milawilila ulipo………...3

3 Ramani ya Tao la Mashariki ikionyesha Milima ya Uluguru……………………….4

4 Mfumo au utaratibu wa kutoa taarifa katika mpango huu……………………….12

## ORODHA YA VIAMBATANISHO

**Kiambatanisho** **Ukurasa**

1 Orodha ya miti katika msitu wa Milawilila…………………………………...…….19

2 Sheria Ndogo……………...…………………………………….…………………..20

## ORODHA YA VIFUPISHO NA KIREFU CHAKE

| | | |
|---|---|---|
| DANIDA | - | Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Denmark |
| DOF | - | Danish Ornithological Foundation (Chama cha Ndege Denmark) |
| HMM | - | Hifadhi ya msitu wa Milawilila |
| NB | - | Nota Benne (Kitu cha kuzingatia) |
| ºC | - | Degrees Centigrade (Nyuzi Joto) |
| W | - | Wilaya |
| WCST | - | Wildlife Conservation Society of Tanzania (Chama cha Kuhifadhi Maliasili na Mazingira Tanzania) |
| UMBCP | - | Uluguru Mountains Biodiversity Conservation Project (Mradi wa |

Kuhifadhi Bioanuwai Milima ya Uluguru)

# SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Mpango huu shirikishi umeandaliwa na kamati ya mpango ambayo imeundwa kutoka katika vijiji vya Milawilila na Mifulu ambavyo vinapakana na msitu wa hifadhi wa Milawilila. Mpango huu umefanyiwa marekebisho na wataalam wa misitu katika ngazi ya wilaya na wa Mradi wa WCST na kupata idhini ya serikali za vijiji husika. Uandaaji wa mpango umehisaniwa na Serikali ya Denmark (kwa kupitia shirika lake la Maendeleo la DANIDA) kwa kupitia DOF na WCST.

Mpango huu umekubalika kuwa chombo cha kusimamia na kutunza msitu wa Milawilila. Mpango huu utajulikana kama **"MPANGO SHIRIKISHI WA USIMAMIZI NA UTUNZAJI WA MSITU WA MILAWILILA WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MOROGORO".**

Mpango huu utafanyiwa majaribio kwa mwaka mmoja, kuanzia Januari 2006 na baada ya kipindi hicho marekebisho ya lazima yatakayojitokeza yatafanyika ili uweze kuwa mpango wa kudumu ambao utakuwa ukifanyiwa marekebisho kila baada ya miaka mitano.


# SEHEMU YA PILI

## 2.0 MAELEZO KUHUSU MSITU

### 2.1 Jina la msitu
Msitu wa hifadhi wa Milawilila

### 2.2 Historia ya msitu.
Msitu wa Milawilila (*Mchoro 1*) ni wa hifadhi ya bioanuwai (viumbe hai) na una namba ya ramani JB2486 (Scale: 1:50,000). Msitu huu unamilikiwa na serikali ya halmashauri ya wilaya ya Morogoro na ulihifadhiwa kisheria na wakoloni mwaka 1914.

### 2.3 Bioanuwai
Msitu wa Milawilila una aina mbalimbali za mimea (*Kiambatanisho 1*) wanyama mbalimbali kama kima, ngedere, mbega, kichakulo, buku mlima, chibase, rukungu, ng'urukuru, kibwene *n.k* na ndege aina ya kulumbizi, chiliku, hondohondo, kunguru, shorwe, ninga, njiwa pori, nyamoto, tongwa, chozi, kanga, *n.k.*, na wadudu mbalimbali. Pia kuna aina mbalimbali za vyura, kinyonga na nyoka. Msitu una aina mbalimbali za wadudu kama inzi, mbung'o, nzige, kipepeo, kumbikumbi, manyigu *n.k.*
Mimea inayopatikana kwenye mabonde inatofautiana kidogo na ile ya maeneo ya mwinuko. Aina ya mimea inayopatikana katika maeneo ya bondeni katika msitu huu ni sawa na ile inayopatikana katika misitu mingine ya maeneo ya mabondeni. Hata hivyo kuna miti michache ambayo inapatikana katika misitu ya nyanda za juu (*mfano, Cepholasphaera usambarensis*).





**Mchoro 1: Msitu wa Hifadhi wa Milawilila**



To Kinole

## 2.4 Eneo uliyopo Msitu

Msitu wa hifadhi wa Milawilila upo katika mwinuko wa kati ya mita 260-400 kutoka usawa wa bahari. Mipaka ya msitu kijiografia ni nyuzi 6º 59´ Kusini na 37º45´Mashariki. Msitu huu uko umbali wa kilometa 60 kusini mwa manispaa ya Morogoro kwa kufuata barabara ya Morogoro – Tawa kupitia Kinole. Vile vile kwa kwa kufuata barabara ya Matombo kupitia Msalabani hadi Tawa ni kilometa 80 kutoka Morogoro. Barabara zote hizi zinapitika kipindi chote cha mwaka. Msitu wa Milawilila upo kama kilometa 7 Mashariki mwa msitu mkubwa wa hifadhi ya serikali kuu wa Uluguru Kaskazini (*Mchoro 2*).





**Mchoro 2: Ramani ya Milima ya Uluguru ikionyesha eneo msitu wa Milawilila ulipo**

## 2.5 Udongo na hali ya hewa

Udongo katika msitu wa Milawilila ni mwekundu kwa upande wa juu na ni mweusi kwa upande wa mabondeni. Kuna sehemu chache ambazo zina udongo wa mfinyanzi. Mvua nyingi (Masika) hunyesha miezi ya Machi hadi Mei kutokana na pepo zinazovuma kutoka bahari ya Hindi. Mvua za vuli hunyesha kuanzia mwezi wa Novemba hadi Januari. Wastani wa mvua zinazonyesha hufikia milimita kati ya 1000-1800 kwa mwaka na wastani wa joto ni kati ya 23 -28ºC.

## 2.6 Uhusiano wa msitu wa hifadhi wa Milawilila na misitu mingine ya milima ya tao la Mashariki

Msitu wa hifadhi wa Milawilila ni mmojawapo ya misitu midogomidogo inayounda misitu ya Uluguru ambayo ni sehemu ya milima ya tao la milima ya mashariki nchini Tanzania. Milima hii inajumuisha milima ya Pare kaskazini na kusini, Usambara mashariki na magharibi, Nguu, Nguru, Ukaguru, Rubeho, Uluguru kaskazini na kusini, Malundwe, Udzungwa na Mahenge. Milima hii iliibuka kwa nguvu za asili miaka milioni 100 iliyopita (*Mchoro* 3). Milima hii ina misitu minene ambayo inasababisha mvua nyingi kutokana na pepo za mashariki ambazo zinavuma kutoka Bahari ya Hindi.




**Mchoro 3: Ramani ya Tao la Mashariki ikionyesha Milima ya Uluguru**

## 2.7 Umuhimu wa Uluguru

Milima ya Uluguru ina umuhimu na sifa za kipekee sio kwa jamii na Tanzania pekee bali hata kwa jamii ya kimataifa pia. Milima hii inahifadhi vyanzo vya maji ambayo yanatumika katika jiji la Dar es Salaam,mji wa Morogoro na sehemu za mikoa ya Pwani

na Morogoro. Pia milima ya Uluguru ni mojawapo ya maeneo 25 yenye wanyama na mimea (bioanuwai) ya kipekee ulimwenguni. Wananchi wanaoishi kando kando ya misitu hii wanapata mahitaji yao kutoka katika misitu hii. Misitu hii pia ni kivutio kikubwa cha watalii licha ya kuwa na umuhimu mkubwa wa kuhifadhi ardhi na kurekebisha hali ya hewa.

Msitu wa hifadhi wa Milawilila haujaathirika sana kutokana na shughuli zinazofanywa na binadamu *mfano* uchomaji moto, kilimo, na uvunaji wa mbao/mazao ya misitu. Ili kuepuka janga hili jamii nzima inayouzunguka msitu huu inaelimishwa na imekubali kuuhifadhi msitu huu na bioanuwai iliyomo pamoja na mazingira yake ambayo ni hazina kubwa kitaifa na kimataifa.

## 2.8 Shughuli za jamii na kiuchumi

Takwimu za vijiji vinavyopakana na msitu wa Milawilila ambazo zilipatikana kutokana na taarifa za vijiji vya Mifulu na Milawilila (*Jedwali 1*).

**Jedwali 1: Takwimu muhimu za vijiji vinavyouzunguka msitu wa Milawilila**

| Kijiji | Idadi ya Watu | Idadi ya Vitongoji | Idadi ya Kaya | Vitongoji vinavyopakana na Msitu | Wastani Wa Mashamba |
|---|---|---|---|---|---|
| Mifulu | Me=911<br>Ke=1098 | 5 | 371 | Limakamwe, Kidai | 7 |
| Milawilila | Me=361<br>Ke=548 | 9 | 235 | Milawilila | 4 |

### 2.8.1 Njia kuu za kiuchumi za vijiji vinavyopakana na msitu wa Milawilila;-

Njia kuu za kiuchumi kwa vijiji vinavyopakana na msitu wa Milawilila ni kama ifuatavyo: -

- Kilimo;
- Ufugaji wa wanyama wadogowadogo kama mbuzi, kondoo, kuku, n.k;
- Biashara ndogondogo;
- Wafanyakazi wachache (walimu na manesi);
- -Dawa za asili.

### 2.8.2 Huduma za jamii katika vijiji

Huduma zinazopatikana katika vijiji vinavyopakana na msitu wa Milawilila ni kama ifuatavyo: -

- Zahanati;
- Shule za msingi;
- Barabara kutoka Morogoro mjini;
- Magenge;
- Misikiti;
- Wakunga wa jadi;
- Waganga wa asili

### 2.8.3 Umuhimu wa msitu wa Milawilila kwa wanakijiji

Umuhimu wa msitu wa Milawilila kwa jamii inayouzunguka ni huu ufuatao: -

- Wanyama kama kivutio cha watalii;

- Dawa za asili kwa ajili ya tiba ya asili na biashara;
- Miti kwa ajili ya kuni, fito za kujengea, mbao, samani, matunda;
- Kamba kwa ajili ya ujenzi, matumizi ya nyumbani na kufungia mizigo;
- Mianzi- biashara (matenga) na ujenzi;
- Uyoga na mboga za asili kwa ajili ya matumizi ya nyumbani;
- Samaki -matumizi ya nyumbani na biashara;
- Viazi vya asili (vikwa) -chakula hasa wakati wa njaa;
- Ndege -kivutio kwa watalii, utafiti, dawa na kitoweo;
- Wadudu –mchwa na kumbi kumbi (chakula na kurutubisha udongo), utabiri wa asili wa msimu (mfano *selenzi*);
- Asali (kidogo) –biashara na dawa;
- Matambiko msitu unatumika kwa matambiko (mila na desturi);
- Uboreshaji wa hali ya hewa;
- Makazi ya bioanuwai (viumbe hai);

#### 2.8.4 Rasilimali zilizopo msituni

Rasilimali zinazopatikana msituni ni: -

- Wanyama mbalimbali (kivutio kwa utalii *mfano* mbega, ndege, n.k.);
- Mazao yasiyo timbao kama vile uyoga, asali, kamba, mboga za asili, mianzi na dawa za kienyeji;
- Wadudu wa aina mbalimbali;
- Madini (mawe, mchanga na udongo, n.k.)
- Mazao yaliyo timbao –mbao, nguzo, na fito.

#### 2.8.5 Shughuli ambazo zinaathiri msitu

Shughuli zinazofanywa na jamii ambazo zinaathiri msitu ni: -

- Uchimbaji wa mizizi na ubanguaji wa magome ya miti kwa ajili ya dawa;
- Ukataji mianzi kwa ajili ya kutengenezea matenga.

# SEHEMU YA TATU

## 3.0 MALENGO YA MPANGO

### 3.1 Lengo la muda mrefu;

Kuhifadhi msitu wa Milawilila kwa njia shirikishi ili kuwepo na matumizi endelevu kwa jamii nzima.

### 3.2 Malengo ya muda mfupi

- Kuandaa utaratibu wa kuinua kipato kwa jamii inayozunguka msitu wa Milawilila;
- Kuboresha bioanuwai (hifadhi ya bioanuwai) iliyopo msituni;
- Kuandaa utaratibu wa kusimamia msitu wa Milawilila kwa njia shirikishi.

### 3.3 Mikakati ya kuendeleza msitu ndani na nje ya msitu.

***Ndani ya msitu***

- Kuendeleza uoto wa asili ndani ya msitu;

- Kudhibiti uchukuaji wa rasilimali za msitu wa Milawilila;
- Kudhibiti kilimo ndani ya msitu;
- Kuweka mabango ya aina mbalimbali yenye ujumbe wa kuhifadhi msitu.

***Nje ya msitu***

- Kuhimiza ufugaji bora wa wanyama *mfano* mbuzi, kondoo, kuku, n.k;
- Kuhimiza upandaji miti ya aina mbalimbali ya asili katika maeneo binafsi ili kukidhi mahitaji;
- Kuweka barabara za kuzuia mioto kuzunguka msitu;
- Kuzuia uandaaji wa mashamba kwa kutumia mioto;
- Kuhimiza ufugaji wa nyuki na samaki ili kuwaletea wananchi kipato;
- Kuhamasisha uanzishwaji wa vitalu vya miti ya asili na matunda;
- Kuhamasisha uanzishwaji wa vikundi vya maendeleo *mfano* mitandao ya wakulima;
- Kuhimiza kilimo bora na endelevu;
- Kuhifadhi vyanzo vya maji na kingo za mito.

## 3.4 Matarajio ya mpango

***Ndani ya msitu***

- Ifikapo mwaka 2010 maeneo yote ya wazi ndani ya msitu yawe na uoto wa asili;
- Ifikapo mwishoni mwa mwezi Januari 2006 uharibifu wa aina yoyote ndani ya msitu uwe umekwisha, *mfano,* uchimbaji wa mizizi na ubanguaji wa magome na ukataji kiholela wa mianzi;
- Ifikapo mwishoni mwa mwezi Januari 2006, mabango yenye jumbe mbalimbali za kuhifadhi yawe yamewekwa maeneo muhimu;
- Ifikapo mwishoni mwa mwezi Januari 2006, vikosi vya doria viwe vimeimarishwa pamoja na kamati za mazingira.

***Nje ya msitu***

- Ifikapo mwaka 2007 wakulima wapatao 200 wa kila kijiji wawe wamepata mafunzo ya kilimo mseto na kilimo bora/endelevu;
- Ifikapo mwaka 2008 watu wote wanaopendelea kufuga nyuki na samaki kutoka kila kijiji kinachozunguka msitu wa Milawilila wawe wamepata mafunzo ya ufugaji nyuki na samaki;
- Ifikapo mwaka 2006 maafisa watendaji wa kata wawe wameitisha mikutano miwili ya ujirani mwema kwa vijiji vyote viwili vinavyouzunguka msitu wa Milawilila;
- Ifikapo mwaka 2007 jamii ya vijiji vyote viwili iwe imehamasishwa juu ya uhifadhi, utunzaji na uendelezaji wa misitu ya asili;
- Ifikapo mwaka 2007 kila kijiji kiwe kimeotesha miti ya asili, 3500 kwa kijiji cha Mifulu na 4500 kwa kijiji cha Milawilila na miti ipandwe kwenye maeneo yote yaliyo wazi, vyanzo vya maji, mito na mipaka ya kijiji na mashamba ya watu;
- Ifikapo mwaka 2008 kila kaya iwe imepanda miti ya asili na ya aina mbalimbali isiyopungua 200;
- Ifikapo mwaka 2007 wananchi wote wa kitongoji ni lazima wawe wamefuga angalau mnyama mmoja;
- Ifikapo mwaka 2008 kila kaya iwe imelima mazao ya biashara kwa ajili ya kujiongezea kipato *kama* migomba na mananasi.

# SEHEMU YA NNE

## 4.0 MFUMO WA USIMAMIZI WA MSITU

### 4.1 Mipaka ya msitu

- Mipaka yote ya msitu wa Milawilila iwekwe alama za kudumu ili iweze kuonekana au kujulikana kirahisi kwa watu wote *mfano* kupanda miti;
- Barabara za moto zitakuwa zikifyekwa mara kwa mara ili kulinda msitu dhidi ya moto;
- Ndani ya msitu hakutakuwepo na mipaka ya usimamizi ya vijiji bali ulinzi wa msitu utafanyika kwa pamoja kwa vijiji vyote viwili.

### 4.2 Usimamizi wa msitu

- Usimamizi wa msitu wa Milawilila utakuwa chini ya kamati za mazingira za kila kijiji ambazo zitawajibika katika halmashauri za vijiji vyao. Kamati hizi zitakuwa na mjumbe mmoja au zaidi (kulingana na idadi ya vitongoji) toka kila kitongoji. Jumla ya wajumbe wasipungue idadi ya wajumbe 10 wakiwepo wanawake wasiopungua 3. Kamati hizi zitachaguliwa na mkutano mkuu wa kijiji na zitakuwa madarakani kwa kipindi cha miaka 5, sambamba na kipindi cha serikali za vijiji. Kamati hizi zitatoa wajumbe 4 kuunda kamati ya uratibu ya msitu wa Milawilila. Wajumbe hawa ni: - Mwenyekiti, katibu na Mweka hazina wa kamati ya kila kijiji watakuwa wajumbe wa kudumu na mjumbe mmoja atakuwa anabadilika kila baada ya mwaka mmoja;
- Kamati za mazingira za vijiji zitakutana mara moja kwa mwezi na kila inapotokea dharura na kutunza kumbukumbu zote za mikutano. Katibu atawakilisha nakala za kumbukumbu katika halmashauri ya kijiji na nakala itolewe kwa kamati ile ya uratibu ya msitu wa milawilila;
- Baada ya wajumbe wa kamati ya mazingira kuchaguliwa wao wenyewe watachagua mwenyekiti, katibu na mweka hazina;
- Idadi ya wajumbe wa kamati ya mazingira wanaotakiwa ili mkutano ufanyike ni lazima wawe zaidi ya nusu ya wajumbe wake;
- Kamati ya mazingira ya kijiji itawajibika kufuatana na taratibu zote zilizowekwa kwa ajili ya kijiji.

### 4.3 Wajibu na madaraka

#### 4.3.1 Muundo wa kamati ya mazingira ya kijiji

Kamati ya mazingira ya kijiji ni kamati ndogo ndani ya kamati ya huduma kwa jamii. Hivyo kamati hiyo itaundwa kwa kuchaguliwa na mkutano mkuu wa kijiji (serikali ya kijiji) na wajumbe hawatapungua 10 na uwiano wa jinsia utazingatiwa.

#### 4.3.2 Wajibu wa kamati za mazingira

Wajibu wa kamati za mazingira ni kama ifuatavyo: -

- Kuhakikisha kwamba walinzi walioteuliwa wanafanya kazi ya doria kama inavyotakiwa na ukaguzi wa msitu utafanyika mara 4 kwa mwezi;
- Kuhakikisha ya kwamba msitu wa Milawilila unatumika kulingana na taratibu za usimamizi zilizowekwa na kukubalika;
- Kuwashughulikia watuhumiwa kufuatana na taratibu, kanuni na sheria za nchi;
- Kuweka kumbukumbu sahihi za masuala yote yanayohusiana na msitu wa Milawilila;
- Kutoa taarifa za utekelezaji wa mpango katika halmashauri ya kijiji kila mwezi;

- Kuhamasisha wananchi kupanda miti nje na ndani ya msitu wa Milawilila na kushiriki kuzima mioto endapo inatokea.

### 4.3.3 Wajibu wa mwenyekiti kamati ya mazingira ya kijiji

- Kuongoza vikao vya kamati ya mazingira;
- Kuhakikisha vikao vya kamati vinaitishwa na maamuzi yanatekelezwa ipasavyo;
- Kuhakikisha katibu anaweka takwimu sahihi kuhusu doria, mapato, vibali, faini na mambo yote yanayohusiana na shughuli za kamati;
- Kuhakikisha walinzi wanashirikiana na kutekeleza wajibu wao;
- Kuhakikisha taarifa na maamuzi ya kikao yanawafikia walengwa;
- Kuwa na mawasiliano ya mara kwa mara na mwenyekiti wa kijiji;
- Kuwasilisha taarifa za kamati za mazingira na kuhudhuria vikao vyote vya kamati ya uratibu wa msitu wa Milawilila;
- Kuhakikisha mweka hazina anaweka takwimu sahihi kuhusu mapato na matumizi ya fedha zote za kamati;
- 

### 4.3.4 Wajibu wa katibu

Kutunza takwimu na kumbukumbu zifuatazo:-

- Kutunza kumbukumbu za kitabu cha mikutano ya mazingira;
- Kutunza kitabu cha doria kuhusu ratiba, mambo yaliyofanyika, uharibifu uliotokea, n.k;
- Kuweka kitabu cha kumbukumbu za watuhumiwa waliokamatwa, faini, tarehe ya faini iliyolipwa, idadi ya stakabadhi iliyotolewa kutokana na faini, n.k;
- Kitabu cha vibali vilivyotolewa, kwa nini, kwa ajili ya nini, lini, idadi ya stakabadhi zilizotolewa;
- Kuwaalika wajumbe kwenye mkutano baada ya kuwasiliana na mwenyekiti wa kamati ya mazingira.

### 4.3.5 Wajibu wa mtunza hazina

- Kutunza vitabu vyote vya fedha;
- Kupokea mapato yote ya fedha na kuwasilisha kwa mtunza fedha wa kamati ya uratibu wa msitu wa Milawilila;
- Kutoa taarifa za fedha za kila mwezi katika kamati ya mazingira ya kijiji.

## 4.4 Muundo na wajibu wa kamati ya uratibu ya msitu wa Milawilila

Wenyeviti, makatibu, waweka hazina na mjumbe mmoja kutoka kila kamati ya mazingira ya vijji vyote viwili vinavyopakana na msitu ndiyo watakaounda kamati ya uratibu (wasimamizi) ya msitu wa Milawilila. Wenyeviti, makatibu na waweka hazina wa kamati za mazingira wanapaswa kuwa wajumbe wa kudumu katika kamati ya uratibu. Wajumbe watakaochaguliwa kuungana na wenyeviti, makatibu na waweka hazina watabadilishwa baada ya mwaka mmoja. Kamati itachagua mwenyekiti, katibu, na mtunza fedha kutoka miongoni mwao.

### 4.4.1 Wajibu wa kamati ya uratibu wa msitu

- Kutoa mgao wa mapato kwa vijiji husika kama itakavyojadiliwa na kukubaliwa katika vikao;

- Itawajibika katika ofisi ya maliasili kata, tarafa na itatoa taarifa zake kwa kamati za mazingira za vijiji husika na kuzifikisha kwenye halmashauri za vijiji;
- Kutoa ushauri katika kamati za mazingira za kila kijiji kuhusu usimamizi wa msitu wa Milawilila na haitahusika katika utendaji;
- Kukutana kila baada ya miezi mitatu au mara nne kwa mwaka;
- Kamati ina uwezo wa kusimamisha au kutoa mgao wa fedha kwa kijiji au vijiji vyote viwili endapo kuna mahitaji ya msingi yamekiukwa na vijiji au kijiji husika;
- Kamati itawasilisha taarifa ya robo mwaka juu ya maendeleo ya usimamizi wa msitu wa Milawilila kwa afisa maliasili wa tarafa;
- Kamati itasimamia ukusanyaji wa mapato kutokana na vyanzo vilivyokubalika tu.

### 4.4.2 Wajibu wa mwenyekiti wa kamati ya uratibu

- Kuongoza vikao na kuhakikisha taarifa zinatolewa na zinawafikia wahusika.

### 4.4.3 Wajibu wa katibu

- Kuitisha vikao, kuratibu na kutunza taarifa zote za vikao vya kamati ya uratibu;
- Kusimamia utendaji kama inavyoelekezwa katika sera mpya ya misitu ya 1998.

### 4.4.4 Wajibu wa mtunza fedha

- Kupokea na kutunza kumbukumbu zote za fedha kutoka kamati zote za mazingira za halmashauri husika;
- Atawajibika kutoa taarifa za mgao wa fedha katika kila kijiji;
- Kufungua akaunti ya kamati ya uratibu wa msitu wa Milawilla na kupeleka fedha zote zitakazo wakilishwa kwake benki;
- Kuandika hundi kwa vijiji vyote kama itakavyoelekezwa na mkutano wa ugawaji wa mapato wa kamati ya uratibu wa msitu wa Milawilila.

## 4.5 Mkaguzi wa mahesabu wa msitu wa Milawilila

Kwa kuwa ukaguzi wa mahesabu ya vijiji unafanywa na halmashauri ya wilaya vivyo hivyo na ukaguzi wa fedha za kamati ya mazingira vijijini zitafanywa na halmashauri ya wilaya

## 4.6 Ulinzi wa msitu

### 4.6.1 Uchaguzi wa walinzi wa doria

Kamati ya ulinzi na usalama ya kijiji ikishirikiana na kamati ya mazingira itachagua walinzi wasiopungua watatu (3) wa doria na watamchagua kiongozi wao ambaye atawajibika kwa kamati ya mazingira ya kijiji. Walinzi hawa wa doria watachaguliwa kwa kuzingatia utendaji wao wa kazi na uaminifu na pia wajue kusoma na kuandika na watakuwa wanabadilishana kila mara kwa mara.

### 4.6.2 Wajibu wa walinzi wa doria.

- Uaminifu katika kazi zote za ndani na nje ya msitu;
- Kiongozi wa doria atapanga ratiba ya doria na atahudhuria mikutano yote ya kamati ya mazingira kutoa taarifa ya hali ya msitu kama mjumbe wa kualikwa na atawajibika kama kamati ya mazingira;
- Doria itafanyika mara moja kwa wiki na wakati wowote kamanda au kiongozi atakapoona kuwa kuna umuhimu wa kufanya hivyo;

- Walinzi hao watatu wanaweza kufanya doria pamoja au kujigawa katika makundi;
- Kutoa taarifa ya matukio kwa kamati za mazingira ya halmashauri ya kijiji na nakala kwa afisa maliasili kata au tarafa;
- Wataongozana na wajumbe wa kamati za mazingira za vijiji walau mara moja kila mwezi kukagua kazi za ulinzi.

### 4.6.3 Wajibu wa wadau

**Wanakijiji (Serikali ya kijiji)**

- Kutunza na kulinda msitu wa Milawilila;
- Kutoa taarifa za uharibifu zinazoonekana katika kamati ya mazingira au katika halmashauri za vijiji;
- Kila mwanakijiji anayelima au aliye jirani na msitu atalinda mpaka wa msitu kwa kupalilia barabara kuzuia moto isiyopungua upana wa mita tatu (3);
- Mwenye shamba atachoma shamba lake baada ya kutoa taarifa kwa kamati ya mazingira na halmashauri ya kijiji.

**Halmashauri ya kjiji**

- Kusimamia na kuhakikisha kuwa shughuli zilizopangwa katika mpango huu zinatekelezwa kikamilifu na kwa wakati uliyopangwa;
- Kuhakikisha kwamba kamati ya mazingira ya kijiji inaimarika na kufanya kazi kikamilifu kwa mujibu wa sheria;
- Kutoa mapendekezo na kutunga sheria za vijiji;
- Kuhakiki na kudhibiti leseni na vibali halali vya kuchukua rasilimali zilizoruhusiwa msituni;
- Kusimamia utekelezaji wa sheria na maagizo mbalimbali yatakayotolewa kutoka ngazi za juu katika kusimamia msitu wa Milawilila;
- Kupitia kamati ya mazingira kupanga waongozaji wageni msituni na kuwapa posho;
- Kukagua msitu mara moja kila baada ya miezi tatu (3).

**Halmashauri ya wilaya**


- Mmiliki wa hifadhi ya msitu wa Milawilila kisheria;
- Kutoa ushauri wa kiufundi na kitaalam kuhusu usimamizi wa msitu wa Milawilila;
- Kuhamasisha jamii juu ya matumizi bora ya ardhi na maliasili zake;
- Kuhamasisha wananchi kuzuia na kushiriki kuzima moto;
- Kusaidia kamati pale yanapotokea matatizo ya kiutendaji;
- Kutoa ushauri katika jamii inayozunguka msitu wa Milawilila kwa shughuli zinazofanyika nje ya msitu;
- Kutoa ushauri kuhusu uundaji wa sheria ndogo na kuzipitisha;
- Kuwa kiungo kati ya serikali kuu na wananchi kuhusu uhifadhi na shughuli za msitu;
- Kukasimu madaraka ya kiutendaji na kukabidhi vijiji husika (ushirikishwaji)

# SEHEMU YA TANO

## 5.0 MFUMO WA KUTOA TAARIFA.

### 5.1 Taarifa za kawaida

Taarifa za kawaida zitafuata utaratibu wa utoaji wa taarifa kama inavyoonyeshwa kwenye mchoro wa 4 hapa chini. Walinzi wa doria watoe taarifa kwa kamati ya mazingira. Kamati ya mazingira itoe taarifa kwa halmashauri ya kijiji na kamati ya uratibu wa msitu wa Milawilila. Kwa mfumo huo, utoaji wa taarifa utaendelea hadi kufikia ngazi za juu kwa utekelezaji.




**Mchoro 4: Mfumo au utaratibu wa kutoa taarifa katika mpango huu**

### 5.2 Taarifa kwa masuala ya dharura

Masuala yote ya dharura kama:-moto taarifa zitatolewa kwa kiongozi yeyote aliye karibu kwa utekelezaji na baadaye taarifa zitaendelea kutolewa kwa kufuata taratibu za ngazi husika.

### 5.3 Taarifa zenye utata

Taarifa zenye utata ni zile zinazowahusisha viongozi, endapo kuna taarifa za uharibifu wa aina yoyote katika msitu na moja kati ya ngazi za uongozi zimehusika, ukipeleka suala hilo katika ngazi hiyo ni wazi halitapewa uzito unaostahili hivyo unaweza kutoa taarifa katika ngazi za juu zaidi.

# SEHEMU YA SITA

## 6.0 KANUNI NA TARATIBU

### 6.1 Utaratibu wa kuingia msituni

- Watu ambao wanaruhusiwa kuingia katika msitu wa Milawilila kwa shughuli mbalimbali za usimamizi kufuatana na taratibu zilizokubalika ni wanavijiji wa Milawilila na Mifulu, maafisa wa maliasili pamoja na viongozi mbalimbali wa serikali kwa kutoa taarifa;
- Watu wengine wote wataruhusiwa kuingia katika msitu wa Milawilila kwa kibali maalum.

### 6.2 Shughuli zilizokatazwa msituni

Shughuli zifuatazo zimekatazwa kabisa kufanyika ndani ya msitu wa Milawilila:-

- Kuanzisha moto ndani ya msitu;
- Kukata aina yoyote ya miti ndani ya msitu;
- Kuharibu uoto wa asili katika sehemu yoyote ya msitu;
- Kuchunga mifugo ndani ya msitu;
- Kuwinda au kutega wanyama ndani ya msitu;
- Utafutaji wa kamba;
- Uchimbaji wa mizizi na ubanguaji wa magome ya miti;
- Kufanya shughuli ya uvuvi ndani ya eneo la msitu;
- Kufanya mambo ya uganga wa kienyeji ndani ya msitu.

### 6.3 Utaratibu wa kuchukua rasilimali msituni

Kwa vile msitu tumeufunga kwa muda basi hakuna rasilimali yoyote itakayochukuliwa msituni hadi hapo utakapofunguliwa au mpango utakapofanyiwa marekebisho.

### 6.4 Huduma za msitu

Huduma zifuatazo zitafanyika ndani ya msitu wa Milawilila zitalipiwa kama inavyoonyeshwa katika Jedwali la 2.

**Jedwali 2: Huduma zitolewazo katika Msitu wa Milawilila na kiasi cha malipo**

| Shughuli | Wahusika | Malipo |
|---|---|---|
| Utafiti bila kuchukua kitu chochote | Wananchi (mtafiti mmoja) | Mtu mmojaTshs. 2,000/= |
| | Wageni (mtafiti mmoja) | Mtu mmoja $ 4 kwa siku |
| Kuingia ndani ya msitu (watalii) | Wageni wakipata waelekezaji | Mtu mmoja kwa siku $ 4 |
| | Wananchi | Mtu mmoja Tshs 3,000/= kwa siku |
| Kuweka kambi ndani ya msitu | Wananchi | Tshs. 2,500/= kwa siku |
| | Watalii | Kila mtu mmoja $4 kwa siku |
| Ziara ya mafunzo | Kwa wageni wote wanaokuja kujifunza ushirikishwaji | Kwa kila kundi Tshs 10,000/= kwa siku |
| Kufanya matambiko (Uganga) | Waganga wa ndani (Milawilila na Mifulu) | Mganga mmoja Tshs. 20,000/= |
| | Waganga toka nje ya vijiji vya Milawilila na Mifulu | Mganga mmoja Tshs. 30,000/= |

### 6.5 Mapato yafuatayo na rasilimali za msituni

Njia za kujipatia kipato ni kama zifuatazo: -

- Kwa kulipia vibali vya kuchukua rasilimali zote na huduma za msitu;
- Mkusanyaji wa mapato yote ni kamati ya mazingira kwa kusimamiwa na halmashauri za vijiji;
- Kamati ya uratibu wa msitu wa Milawilila itafungua akaunti Benki katika benki ya Wakulima ya Kinole. Akaunti hiyo itafunguliwa kwa jina la “**KAMATI YA URATIBU YA MIFUMILA**”;
- Watia sahihi katika akaunti hii watakuwa watatu ambao ni: -
  - (i) Mweka Hazina wa kamati ya uratibu msitu wa Milawilila;
  - (ii) Mwenyekiti wa kijiji cha Mifulu;
  - (iii) Mwenyekiti wa kijiji cha Milawilila.

## SEHEMU YA SABA

### 7.0 NAMNA YA KUWASHUGHULIKIA WAHALIFU.

### 7.1 Utaratibu

Uhalifu dhidi ya msitu utashughulikia kama ifuatavyo: -

i) Walinzi wakimkamata mtuhumiwa watampeleka kwa mwenyekiti au katibu wa kamati ya mazingira ya kijiji endapo atakiri kosa kwa maandishi, mtuhumiwa atatozwa faini papo hapo na mwenyekiti au katibu lakini pakiwepo na shuhuda angalau mjumbe mmoja wa kamati ya mazingira;
   - Mtuhumiwa atakapokataa kwa maandishi atafikishwa katika kamati ya mazingira ambako atapangiwa muda na tarehe ya kujibu tuhuma. Endapo mtuhumiwa hatakubali kosa kamati ya mazingira itatoa taarifa juu ya suala husika kwa mwenyekiti au Afisa mtendaji wa kijiji. Hawa nao wakishindwa kupata ufumbuzi, mwenyekiti wa kamati ya mazingira pamoja na mwenyekiti wa kijiji watapeleka kesi mahakamani;
   - Mlinzi wa msitu haruhusiwi kutoza faini kwa mhalifu, iwapo mlinzi/walinzi watagundulika wamefanya hivyo wataitwa mbele ya kamati ya mazingira ya kijiji na kujibu tuhuma, akibainika ana hatia anaweza kufutwa kuwa mlinzi au kumtoza faini;
   - Watuhumiwa watalazimika kulipa faini (fedha taslimu) kwa kila kosa kulingana na viwango vilivyowekwa;

ii) Mazao ya msitu yaliyokamatwa yatataifishwa na yatawekwa katika ofisi ya halmashauri ya kijiji kwa ajili ya hatua zaidi;

iii) Mtuhumiwa akikiri kosa faini italipwa kwa mtunza fedha ambaye atanakili kiasi kilicholipwa, tarehe na kutoa stakabadhi kwa mtuhumiwa. Nakala ya stakabadhi itatunzwa katika kitabu cha stakabadhi. Namba ya stakabadhi itaandikwa katika kitabu cha watuhumiwa na faini, pia fedha zitapelekwa kwa mtunza fedha wa kamati ya uratibu ya msitu wa Milawilila. Mali iliyotaifishwa nayo ikishauzwa fedha atapelekewa mtunza fedha;

iv) Pamoja na kutoza faini kifungu 167(3) cha sheria ya serikali za mitaa namba (7 ya mwaka 1982) kinaipa uwezo kamati ya mazingira ya kijiji kutoza faini.

### 7.2 Fidia

Kufidia gharama za uharibifu uliyofanywa ndani ya msitu, kiwango kitawekwa kwa kulingana na uharibifu uliofanyika. Mwenyekiti wa kamati ya mazingira ya kijiji wakiwepo wajumbe wa kamati ya mazingira wasiopungua 5 watakagua uharibifu uliosababishwa na mtuhumiwa na afisa misitu anaweza kuombwa kufanya tathimini.

### 7.3 Kulipa gharama

- Mtuhumiwa atahusika pamoja na fidia ya uharibifu uliofanyika kulipa gharama zingine zilizo husika wakati wa tukio husika;
- Kamati ya mazingira ya kijiji inaweza ikaamua kutoa adhabu kwa mtuhumiwa ya kufanya kazi katika msitu wa Milawilila. Kama vile kusafisha au kupanda miti kwenye mipaka na taarifa kupelekwa katika kamati ya uratibu ya msitu wa Milawilila. Mjumbe wa halmashauri ya kijiji au wa kamati au mlinzi anapothibitika kufanya uharibifu, atatozwa faini ya kawaida na faini ya uwajibikaji kwa kushindwa kutekeleza wajibu wake.

### 7.4 Viwango vya faini

#### 7.4.1 Uchomaji mkaa au upasuaji mbao

Mtu akikamatwa anachoma mkaa au kupasua mbao ndani ya msitu wa Milawilila atalipa faini ya Tshs. 65,000/= na kutaifishwa mali na vifaa atakavyoshikwa navyo.

#### 7.4.2 Kuanzisha moto msituni

- Faini ya kuanzisha moto ndani ya msitu wa Milawilila ni kati ya Tshs. 20,000/= na 50,000/=;
- Faini ya kuchoma moto msitu wa Milawilila itakuwa kati ya Tshs. 50,000/= na 100,000/=.

#### 7.4.3 Kutokuwa na kibali kwa shughuli zinazolipiwa ushuru

- Kukata mijengo, fito bila kibali faini ni Tshs. 10,000/= na mali atakayo kamatwa nayo na vifaa vitakuwa mali ya kijiji au vijiji vya Milawilila na Mifulu;
- Kukata mianzi bila kibali faini yake ni Tshs. 30,000/= na mali atakayokamatwa nayo na vifaa vitakuwa mali ya vijiji vya Milawilila na Mifulu;
- Kukata nyasi, kamba, kuchuma matunda, kuchimba viazi vya asili (vikwa) faini yake ni Tshs. 5,000/= na mali atakayokamatwa nayo na vifaa kuchukuliwa na vijiji vya Milawilila na Mifulu;
- Kubangua magome ya miti na uchimbaji wa mizizi bila kibali faini yake ni Tshs. 20,000/= na mali itataifishwa na kuwa mali ya vijiji vyote viwili;
- Kuvua samaki katika eneo la msitu bila kibali faini itakuwa ni Tshs. 10,000/= kwa anayevua bila kutumia sumu na Tshs. 30,000/= kwa anayetumia sumu na nyara/vifaa kutaifishwa;
- Kwa mtu yeyote atakayeingia msituni akiwa na shoka, panga nyengo, msumeno, nyundo faini yake ni Tshs 50,000/= na vifaa vyake vyote alivyokuwa anatumia pamoja na mali kuchukuliwa na vijiji husika;
- Mgeni mtanzania kuingia katika msitu wa Milawilila bila kibali faini yake iwe Tshs. 30,000/=;
- Kwa mgeni asiyekuwa mtanzania kama ataingia msituni bila kibali atafikishwa kwenye vyombo vya dola na kufunguliwa mashitaka;

- Kufanya matambiko msituni kwa ajili ya tiba ya asili (uganga wa kienyeji) bila kibali faini itakuwa kati ya Tshs. 30,000/= na 35,000/=;
- Kuwinda au kutega wanyama msituni bila kibali faini iwe Tshs 15,000/=;
- Kuchunga mifugo ndani ya msitu wa Milawilila faini yake ni Tshs 5,000/= kwa kila mfugo;
- Kuharibu uoto wa asili msituni kwa kulima au kufyeka faini yake ni Tshs. 5,000/=;

#### 7.4.4 Kutokuwa na kibali kwa shughuli zisizolipiwa ushuru
Faini yake ni Tshs. 5,000/= pamoja na mali kutaifishwa na vijiji husika.

#### 7.4.5 Faini ya kutowajibika kwa viongozi
Faini ya kutowajibika kwa viongozi iwe sh 5,000/= kwa kila kosa atakalofanya.

#### 7.4.6 Mtoa taarifa ya uharibifu
Mtoa taarifa atakayetoa taarifa ya aina yoyote ya uharibifu itakayowezesha mtuhumiwa kukamatwa atastahili kupewa asilimia 10 ya pato litakalopatikana na mali hiyo.

***NB: Kwenye matukio kama haya ya kutoza faini kamati ya mazingira itaweka fedha hizo kwenye akaunti ya Kamati ya Uratibu ya MIFUMILA na itatoa taarifa kwa halmashauri za vijiji husika***

## SEHEMU YA NANE

### 8.0 MAPATO NA MATUMIZI YATOKANAYO NA FAINI

i) Mapato yote yatokanayo na faini na ada yatatolewa taarifa kwenye halmashauri ya kijiji;

ii) Matumizi ya mapato yatakuwa kwa ajili ya shughuli ya kuhifadhi msitu wa Milawilila na maendeleo ya kijiji. Matumizi yanaweza yakahusisha mambo yafuatayo: -

**a) Umuhimu wa kwanza.**
- Ununuzi wa vifaa vya ofisi na vitabu vya kutunzia taarifa;
- Ununuzi wa vifaa vya ulinzi *mfano* mabuti, makoti, n.k;
- Gharama za usafiri kwa kamati na wajumbe wengine watakaohusishwa;
- Uendelezaji wa msitu wa hifadhi wa Milawilila;
- Posho kwa walinzi kama motisha wa kazi zao;
- Utengenezaji wa vipeperushi kuhusu msitu wa Milawilila kwa ajili ya wageni.

**(b) Umuhimu wa pili**
- Shughuli mbalimbali za maendeleo ya jamii au kijiji;

**Suala Muhimu la kuzingatia**

Matumizi yote lazima yapangiwe bajeti na yapitishwe na halmashauri ya kijiji na kupitishwa na mkutano mkuu wa serikali ya kijiji. Kwa kuzingatia umuhimu wa shughuli zenyewe, shughuli zote za dharura za kijiji zinaweza kupitishwa na halmashauri ya kijiji na baadaye kutoa taarifa kwenye mkutano mkuu wa kijiji.

iii) **Mgao wa mapato**

Mapato yote yatakayopatikana kutokana na maliasili katika msitu wa Milawilila yatagawiwa sawa katika vijiji husika ambavyo ni Milawilila na Mifulu.

# SEHEMU YA TISA

## 9.0 UFUATILIAJI

### 9.1 Juhudi zitakazofanywa

- Ili kupima ufanisi wa mpango huu, ufuatiliaji utafanyika kila mwaka kwa muda utakaopangwa na kamati ya Uratibu ya msitu wa Milawilila ukiongozwa na Afisa misitu wa wilaya, itakagua hali ya msitu wa Milawilila na kutoa taarifa za matukio na mapendekezo kwenye kamati za mazingira za vijiji;
- Afisa misitu wa wilaya baada ya kukagua atatoa taarifa yake yenye mapendekezo ya namna ya kutunza msitu wa Milawilila kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya na nakala itolewe kwa Afisa Maliasili wa Wilaya;
- Kamati za mazingira za vijiji zitakusanya taarifa zote za msitu wa Milawilila kama ifuatavyo kwa kila mwaka na kuzitolea taarifa kwa halmashauri za vijiji, mkutano mkuu wa kijiji na Afisa Misitu Wilaya na kupeleka nakala Halmashauri ya Wilaya: -
  i) Matukio ya moto;
  ii) Idadi ya tuhuma;
  iii) Idadi ya watuhumiwa watakaokamatwa;
  iv) Vibali vilivyotolewa na aina ya mazao yaliyohusishwa;
  v) Taarifa ya mapato na matumizi kutokana na vibali na faini zilizotolewa;
  vi) Taarifa juu ya tathimini inayohusu mabadiliko ya msitu;
  vii) Matatizo yaliyojitokeza katika kipindi cha mwaka mmoja.

### 9.2 Viashirio vya mafanikio

#### 9.2.1 Kuboreka kwa hali ya msitu wa Milawilila

Hali ya msitu inaboreka kama itakavyoonekana kupitia viashiria vifuatavyo: -

- Kuongezeka kwa uoto wa asili hasa kwa maeneo yaliyokuwa wazi ndani ya msitu;
- Idadi ya wanyamapori na ndege kuongezeka ndani na nje ya msitu;
- Kupungua kwa moto ndani na nje ya msitu;
- Vyanzo vya maji kuongezeka na nje kuwa na uoto wa asili;
- Kuongezeka kwa miti ya asili nje ya msitu;
- Ufugaji wa nyuki na samaki kuongezeka vijijini;
- Kupunguwa kwa idadi ya watu kuingia msituni kuchukua mahitaji;
- Ubanguaji wa magome ya miti na uchimbaji wa mizizi msituni unapungua;
- Uwazi na ukweli wa utoaji wa taarifa juu ya matukio ndani ya msitu unaongezeka;
- Kupungua kwa kesi zinazopelekwa mahakamani zinazohusu uharibifu wa mazingira;

#### 9.2.2 Usimamizi wa msitu kuwa hai

Usimamizi wa msitu utaashiria kuwa hai kwa yafuatayo: -

- Mikutano ya mara kwa mara ya kamati ya uratibu ya msitu wa Milawilila na zile za mazingira za vijiji;

- Kamati za mazingira za vijiji zinaheshimika na wanakijiji;
- Walinzi wanaendelea na doria, wanatoa taarifa sahihi na wanakubali kusimamiwa;
- Utaratibu wa vibali na kadhalika unafuatwa na kuendelezwa;
- Taarifa zinatuzwa kama ilivyopangwa;
- Mipaka inawekwa wazi na alama zinatunzwa;
- Watuhumiwa wanakamatwa;
- Mapato yatokanayo na faini na vibali yananakiliwa vizuri na matumizi yanaenda sawa na mpango huu;
- Watu kutoka nje wanaheshimu sheria katika mpango juu ya usimamizi wa msitu wa Milawilila;
- Urahisi wa kupatikana kwa nyaraka na mihutasari ya vikao mbalimbali katika ofisi za vijiji husika ambavyo ni Milawilila na Mifulu;
- Hakuna migongano ya kiuongozi ndani ya kamati au kijiji kuhusiana na shughuli za usimamizi wa msitu wa Milawilila;
- Wananchi wanathamini shughuli za usimamizi za msitu wa Milawilila na wanatoa ushirikiano kwa kamati za mazingira na serikali zao za vijiji;
- Utekelezaji wa sheria na kanuni kwa kila anayekosa unakuwa wazi na unafuatwa.

# VIAMBATANISHO

## *Kiambatanisho Namba 1*

## Orodha ya miti katika msitu wa Milawilila

| Na. | Jina la Kilatini | Kiswahili/Kiluguru | Familia |
|---|---|---|---|
| **1** | ***Acacia schweinfurthii*** | **Lugogandima** | Mimosaceae |
| **2** | ***Afzelia quansensis*** | **Mkongo** | Papilionaceae |
| **3** | ***Albizia gummifera*** | **Mkenge** | Mimosaceae |
| **4** | ***Anthocleista grandiflora*** | **Mnguva** | Loganiaceae |
| **5** | ***Antiaris toxicaria*** | **Mbila** | Moraceae |
| **6** | ***Aoranthe penduliflora*** | | Rubiaceae |
| **7** | ***Blighia unijugata*** | **Mzindanguruises** | Sapindaceae |
| **8** | ***Bombax rhodognaphalon*** | **Msufi-pori** | Bombacaceae |
| **9** | ***Breonardia salicina*** | **Mgwena** | Rubiaceae |
| **10** | ***Bridelia micrantha*** | **Mwiza** | Euphorbiaceae |
| **11** | ***Calvalhoa campanulata*** | **Mberumberu** | Apocynaceae |
| **12** | ***Ceiba pentandra*** | **Msufi** | Bombacaceae |
| **13** | ***Celtis gophophylla*** | | Ulmaceae |
| **14** | ***Cephalosphaera usambarensis*** | | Myrist. |
| **15** | ***Dracaena sp.*** | **Msenene** | Dracaenaceae |
| **16** | ***Erythrophleum suaveolens*** | **Mkarati** | Caesalpiniaceae |
| **17** | ***Ficus sur*** | **Mkuyu** | Moraceae |
| **18** | ***Ficus thronningii*** | **Msamvu** | Moraceae |
| **19** | ***Funtumia africana*** | **Kilimboti(S)** | Apocynaceae |
| **20** | ***Harungana madagarcariensis*** | **Mtunu** | Guttiferae |
| **21** | ***Khaya Anthotheca*** | **Mkangazi** | Meliaceae |
| **22** | ***Macaranga capensis*** | **Msoto** | Eughorbiaceae |
| **23** | ***Memecylon brenani*** | | Melas |
| **24** | ***Mesogyne insignis*** | **Mkuke** | Moraceae |
| **25** | ***Milicia excelsa*** | **Mvule** | Moraceae |
| **26** | ***Myrianthus arboreus*** | **Mgida** | Moraceae |
| **27** | ***Oryla latifolia*** | **Kilanzilanzi** | Gramineae |
| **28** | ***Parkia filcoidea*** | **Mkundi** | Mimosaceae |
| **29** | ***Quassia undulata*** | **Milawilila** | Simaroubaceae |
| **30** | ***Rinorea ilicifolia*** | | Velloziaceae |
| **31** | ***Rothmannia manganjae*** | | Rubiaceae |
| **32** | ***Rutidea fuscescens*** | | Rubiaceae |
| **33** | ***Rytigynia Sp*** | | Rubiaceae |
| **34** | ***Schizozygia coffaeoides*** | | Apocynaceae |
| **35** | ***Sorindeia madagascariensis*** | **Mhilihili** | Anacardiaceae |
| **36** | ***Synsepalum brevipes*** | **Mkozongo** | Sapotaceae |
| **37** | ***Synsepalum seraciferum*** | **Mkumbulu** | Sapotaceae |
| **38** | ***Tabernaemontana pachysiphon*** | **Mlengolengo mkulu** | Apocynaceae |
| **39** | ***Tetrapleura tetraptera*** | | Mimosaceae |
| **40** | ***Trema orientalis*** | **Mbefu** | Ulmaceae |
| **41** | ***Triacola funifera*** | | Menis. |
| **42** | ***Trichilia volkensii*** | | Meliaceae |
| **43** | ***Trilepsium madagaseariense*** | **Nyakititu** | Moraceae |
| **44** | ***Uapaca sansibarica*** | | Euphorbiaceae |
| **45** | ***Vitex domiana*** | **Mfulu** | Verbenaceae |
| **46** | ***Voacanga africana*** | **Mlengolengo-mdogo** | Apocynacea |

## *Kiambatanisho Namba 2*

*Sheria hizi hazitatumika hadi zimepitishwa na Halmashauri ya Wilaya badala yake sheria mama za uhifadhi za misitu zitatumika.*

## SHERIA ZA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA HALMASHAURI) NA 7 YA 1982 KANUNI (SERIKALI ZA VIJIJI) SHERIA NDOGO,

**Zilizotungwa chini ya vifungu 163 na 167 na marekebisho yake kifungu 38 cha 1998.**

***Jina na Kusomeka***

1 Sheria ndogo hizi zitajulikana kama sheria ndogo za uhifadhi wa msitu wa Milawilila kwa vijiji vya Milawilila na Mifulu zilizotungwa na serikali za vijiji vya Milawilila na Mifulu kwa lengo la kutunza, kuulinda na kuuendeleza msitu wa hifadhi wa Milawilila.

***Tafsiri***

2 Maana ya maneno au vifungu vya maneno yatakayojitokeza mara kwa mara katika sheria hizi.

***Mpango shirikishi***

Maana yake ni mpango wa usimamizi uliotayarishwa na wajumbe kutoka uongozi na kamati za mazingira za vijiji vya Mifulu na Milawilila kwa ajili ya Hifadhi ya Msitu wa Milawilia (HMM) wenye mwelekeo wa kulinda, kutunza, na kusimamia HMM ambao ulijadiliwa na serikali za vijiji na kukubaliwa na Mkurugenzi wa Wilaya ya Morogoro.

***Mkutano mkuu wa kijiji***

Maana yake ni mkutano wa hadhara wa wanakijiji wote wa vijiji vya Mifulu na Milawilila.

***Kamati ya***
**Uratibu ya msitu**

Maana yake ni kamati ya kuratibu na kuunganisha masuala yote ya ulinzi, utunzaji na uendelezaji wa HMM iliyoundwa kutoka katika vijiji vya Mifulu na Milawilila vinavyopakana na msitu huo.

**Walinzi wa doria**

Maana yake ni watu walioteuliwa na kamati za mazingira za vijiji vya Mifulu na Milawilila kwa ajili ya kulinda, kutunza na kuendeleza HMM.

***Halmashauri ya Kijiji***

Maana yake ni Halmashauri ya kijiji cha Mifulu na Milawiliala yenye wajumbe wasiopungua 15 na wasiozidi 25 kwa kila kijiji.

***Mahakama***

Maana yake ni mahakama ya mwanzo au mahakama ya wilaya

***Madhumuni***

3(1) Sheria ndogo hizi zinaweka bayana masharti yaliyokubaliwa na kuidhinishwa na serikali za Mifulu na Milawilila kwa ushauri kutoka kwa wataalamu toka Halmashauri ya wilaya Morogoro na Mradi wa Kuhifadhi Bioanuwai na Maliasili za Milima ya Uluguru kwa lengo la kulinda na kutunza HMM uliopo katika vijiji vya Mifulu na Milawilila.

3(2) Masharti haya yamejadiliwa, kukubalika na kupitishwa na serikali za vijiji vya Mifulu na Milawilila na kuridhiwa na Mkurugenzi wa Wilaya ya Morogoro.

***Meneja Mteule***

3(3) Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro amezishirikisha serikali za vijiji vya Mifulu na Milawilila katika uangalizi na uendelezaji wa HMM.

3(4) Kamati ya Uratibu wa Msitu imechaguliwa kutoka vijiji vya Mifulu na Milawilila kuwa mratibu wa usimamizi wa mpango huu kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa mpango katika utunzaji wa HMM kwa niaba ya wanakijiji wa Mifulu na Milawilila.

3(5) Bwana miti yeyote wa idara ya misitu katika wilaya wakati wowote kwa taarifaanaruhusiwa kufanya ukaguzi katika HMM na kutoa mapendekezo au ushauri kwa kamati ya uratibu wa msitu na kamati za mazingira za vijiji na inapasa kamati kuchukua ushauri huo au mapendekezo hayo na kufanyia kazi.

***Kamati Ya Mazingira***

4(1) Kamati za mazingira za vijiji vya Mifulu na Milawilila zitachaguliwa kufuata taratibu zilizoelezwa katika mwongozo wa ushirikishwaji. Itakuwa na wajumbe wasiopungua kumi (10) wakiwepo wanawake wasiopungua watatu (3) na itawahusisha wawakilishi kutoka katika kila kitongoji.

4(2) Kamati hizi baada ya kuchaguliwa na serikali ya kijiji, wajumbe watachagua Mwenyekiti, Katibu na Mweka Hazina miongoni mwao.

4(3) Wakati kamati ikiwa kwenye madaraka na patakapotokea malalamiko kutoka kwa yeyote yule kuhusu mwanakamati yeyote, Mwenyekiti, katibu au Mweka Hazina ni budi Mwenyekiti wa kijiji na halmashauri yake achukue hatua za kuchunguza hali hiyo na kuchukua hatua za haraka inavyopasa.

4(4) Katibu ataandika taarifa za vikao vya kamati na kutunza kumbukumbu za vikao hivi. Idadi ya wajumbe wa kamati ya mazingira wanaotakiwa ili kikao kifanyike ni lazima wasipungue nusu ya wajumbe wake.

4(5) Kwa nafasi zao kijijini wenyeviti na maafisa watendaji wa vijiji vya Mifulu na Milawilila wanaweza kuhudhuria katika vikao vya kamati ya uratibu wa msitu wa HMM.

***Wajibu Wa Kamati***
***Ya Uratibu Ya HMM***

5(1) Itawajibika katika ofisi ya maliasili kata , tarafa na itatoa taarifa zake kwa halmashauri za vijiji kupitia kamati za mazingira za vijiji husika.

5(2) Kutoa mgao wa mapato kwa vijiji husika kama itakavyojadiliwa na kukubaliwa katika vikao

5(3) Kutoa ushauri katika kamati za mazingira za kila vijiji kuhusu usimamizi wa msitu wa Milawilila na haitahusika katika utendaji wa moja kwa moja.

5(4) Kukutana mara nne (4) kwa mwaka

5(5) Kamati ina uwezo wa kusimamisha au kutokutoa mgao wa fedha kwa muda kijiji au vijiji vyote viwili endapo utendaji wa kazi wa vijiji husika hauridhishi.

5(6) Kamati itawasilisha taarifa ya robo mwaka juu ya maendeleo ya usimamizi wa msitu wa Milawilila kwa afisa maliasili wa kata na tarafa.

***Taarifa***

6(1) Kamati za mazingira za kila kijiji zitatoa taarifa za maendeleo yake kila mwezi kwa Halmashauri za vijiji husika na kupeleka nakala kwa Afisa Mtendaji wa Kata, Katibu Tarafa, Afisa Misitu Tarafa na kamati ya Uratibu ya HMM.

***Uwekaji Kumbukumbu***

7(1) Kamati za mazingira zitaweka kumbukumbu zifuatazo: -

- Vikao vyote vinavyofanyika kwenye kitabu cha kumbukumbu za mikutano;
- Tarehe/siku za kufanya doria kwenye kitabu cha doria;
- Watu waliofanya uhalifu, faini walizotozwa na walizolipa kwenye kitabu cha uhalifu na faini;
- Vibali vilivyotolewa kwenye kitabu cha vibali;
- Mapato na matumizi kwenye kitabu cha mapato na matumizi;
- Kumbukumbu za kesi zote na matukio mengine.

***Kutunza Mapato***

8(1) Kamati ya uratibu wa msitu wa Milawilila itabidi kufungua akaunti benki kwa ajili ya kuweka fedha zote zinazotokana na usimamizi wa msitu HMM.

8(2) Akaunti hii itakuwa na watu watatu watakaoweka saini na hataruhusiwa kuchukua fedha bila saini ya watu watatu (3) kwa pamoja na kumbukumbu za kikao cha kamati ya uratibu ya HMM.

8(3) Taarifa ya mapato na matumizi itatolewa katika mkutano mkuu wa kijiji kila baada ya miezi sita.

***Matumizi Ya Fedha Zitokanazo Na Maliasili***

9(1) Mapato yote yatokanayo na ada na faini, yatatolewa taarifa kwenye mikutano mikuu ya vijiji.

9(2) Matumizi ya mapato yatakuwa kwa ajili ya shughuli za kuimarisha HMM na maendeleo ya vijiji husika (Mifulu na Milawilila). Matumizi yanaweza kuhusisha mambo yafuatayo: -

**(i) Umuhimu wa kwanza**

- Ununuzi wa vifaa vya ofisi na vitabu vya kutunzia taarifa;
- Ununuzi wa vifaa vya ulinzi *mfano* mabuti, makoti, n.k;
- Gharama za usafiri kwa kamati na wajumbe wengine watakaohusishwa;
- Uendelezaji wa msitu wa hifadhi wa Milawilila;
- Posho kwa walinzi kama motisha wa kazi zao;
- Utengenezaji wa vipeperushi kuhusu msitu wa Milawilila kwa ajili ya wageni.

**(ii) Umuhimu wa pili**

- Shughuli mbalimbali za maendeleo ya jamii au kijiji.

NB: Shughuli zote za dharura; halmashauri ya kijiji inaweza kupitisha na kutoa taarifa kwenye mkutano mkuu wa kijiji. Taarifa za matukio mbalimbali zitolewe kwa afisa misitu kata au tarafa, na nakala itolewe kijijini. Matumizi yote lazima yapate kibali toka Halmashauri ya kijiji na kupitishwa na mkuu wa kijiji kwa kuzingatia umuhimu wa shughuli zenyewe.

***Masharti Ya Matumizi***

10(1) Mwanakijiji au mtu yeyote anayetumwa kikazi na halmashauri au serikali ya kijiji anaruhusiwa kuingia kwenye HMM.

***Ulinzi Wa Msitu***

11(1) Kuchagua walinzi wa doria

11(1),(i) Kamati ya ulinzi na usalama ya kijiji ikishirikiana na kamati ya mazingira itachagua walinzi wasiopungua watatu (3) wa doria na watamchagua kiongozi wao ambaye atawajibika kwa kamati ya mazingira ya kijiji;

11(1),(ii) Walinzi hawa wa doria watachaguliwa kwa kuzingatia yafuatayo: -

- Utendaji wao wa kazi;
- Uaminifu;
- Wajue kusoma na kuandika;
- Wawe wanamazingira wazuri.

11(2) Wajibu wa Walinzi wa doria

11(2), (i) Uaminifu katika kazi zote za ndani na nje ya msitu;

11(2), (ii) Kiongozi wa doria atapanga ratiba ya doria na atahudhuria mikutano yote ya kamati ya mazingira kutoa taarifa ya hali ya msitu kama mjumbe wa kualikwa na atawajibika kama kamati ya mazingira;

11(2), (iii) Doria itafanyika mara moja kwa wiki na wakati wowote kamanda au kiongozi atakapoona kuwa kuna umuhimu wa kufanya hivyo. Walinzi hao watatu wanaweza kufanya doria pamoja (kwa vijiji vyote) au kujigawa katika makundi (kwa maana ya kila kijiji kufanya pekee yao);

11(2), (iv) Kutoa taarifa ya matukio kwa kamati za mazingira ya halmashauri ya kijiji na nakala kwa afisa maliasili kata au tarafa;

***Vitendo Vilivyozuiliwa Na Kupigwa Marufuku***

12 (1) Shughuli zifuatazo zimepigwa marufuku kufanyika ndani ya HMM: -

- Kuanzisha moto ndani ya msitu;
- Kukata aina yoyote ya miti ndani ya msitu;
- Kuharibu uoto wa asili katika sehemu yoyote ya msitu;
- Kuchunga mifugo ndani ya msitu;
- Kuwinda au kutega wanyama ndani ya msitu;
- Utafutaji wa kamba;
- Uchimbaji wa mizizi na ubanguaji wa magome ya miti;
- Kufanya shughuli ya uvuvi ndani ya eneo la msitu;
- Kufanya mambo ya uganga wa kienyeji ndani ya msitu.

***Vitendo Vinavyohitaji Kibali Na Malipo***

13(1) Kwa sasa hivi msitu umefungwa kwa muda hivyo hakuna rasilimali yoyote itakayochukuliwa msituni hadi hapo utakapofunguliwa au mpango utakapofanyiwa marekebisho. Hata hivyo hali ya msitu ndiyo itakayoruhusu uvunaji kwa kutumia vibali kwa sasa msitu umeaathirika kiasi.

13(2) Huduma za msitu
Huduma zote ndani ya HMM zitalipiwa kama zilivyoonyeshwa kwenye mpango.

***Utaratibu Wa Kushughulikia Wahalifu***

14(1) Utaratibu

14(2) Uhalifu dhidi ya msitu utashughulikiwa kama ifuatavyo: -

14(2), (i) Walinzi wakimkamata mtuhumiwa, watampeleka kwa mwenyekiti au katibu wa kamati ya mazingira ya kijiji. Akikiri kosa kwa maandishi, mtuhumiwa atatozwa faini papo hapo na mwenyekiti au katibu lakini pakiwepo ushuhuda angalau mjumbe mmoja wa kamati ya mazingira.

14(2),(ii) Mtuhumiwa anapokataa kwa maandishi atafikishwa katika kamati ya mazingira ambako atapangiwa muda na tarehe ya kujibu tuhuma. Akikataa kosa kamati ya mazingira itatoa taarifa juu ya suala husika kwa mwenyekiti au Afisa Mtendaji wa kijiji kwa maana ya halmashauri ya kijiji. Hawa nao wakishindwa

kupata ufumbuzi, mwenyekiti wa kamati ya mazingira pamoja na mwenyekiti wa kijiji watapeleka kesi mahakamani

14(2),(iii) Mlinzi wa msitu haruhusiwi kutoza faini kwa mhalifu, iwapo mlinzi/walinzi watagundulika wamefanya hivyo wataitwa mbele ya kamati ya mazingira ya kijiji na kujibu tuhuma, akibainika ana hatia anaweza kufutwa kuwa mlinzi au kumtoza faini.

14(2),(iv) Watuhumiwa watalazimika kulipa faini (fedha taslimu) kwa kila kosa kulingana na viwango vilivyowekwa.

(a) Mazao ya msitu yaliyokamatwa yatataifishwa na yatawekwa katika ofisi ya halmashauri ya kijiji kwa ajili ya hatua zaidi ambazo zitalenga kukinufaisha kijiji siyo mtu binafsi;

(b) Mtuhumiwa akikiri kosa faini italipwa kwa mtunza fedha ambaye atanakili kiasi kilicholipwa, tarehe na kutoa stakabadhi kwa mtuhumiwa. Nakala ya stakabadhi itatuzwa katika kitabu cha stakabadhi. Namba ya stakabadhi itaandikwa katika kitabu cha watuhumiwa na faini, pia fedha zitapelekwa kwa mtunza fedha wa kamati ya uratibu ya msitu wa Milawilila;

(c) Pamoja na kutoza faini kifungu 167(3) cha sheria ya serikali za mitaa namba (7 ya mwaka 1982) kinaipa uwezo kamati ya mazingira ya kijiji kutoza faini.

***Kiasi Cha Faini***

15(1) Viwango vya Faini

**Viwango vya faini kwa makosa mbalimbali ni kama ifuatavyo:-**

15 (1), (1) Uchomaji mkaa au upasuaji mbao

Faini ni Tshs. 65,000/= na kutaifishwa vifaa na mali yote.

15 (1), (2) Kuanzisha moto msituni

(i) Kuanzisha moto ndani ya msitu faini ni kati ya Tshs. 20,000/= na 50,000/=.

(ii) Kuchoma moto msitu ni kati ya Tshs. 50,000/= na 100,000/=.

**Kutokuwa na kibali kwa shughuli zinazolipiwa ushuru**

15 (1), (3) Kukata mijengo, fito bila kibali faini ni Tshs. 10,000/= na mali atakayo kamatwa nayo itakuwa mali ya kijiji.

15 (1), (4) Kukata mianzi bila kibali faini yake ni Tshs. 30,000/= na mali atakayokamatwa nayo itakuwa mali ya vijiji vya Milawilila na Mifulu.

15 (1), (5) Kukata nyasi, kamba, kuchuma matunda, kuchimba viazi vya asili (vikwa) faini yake ni Tshs. 5,000/= na vifaa na mali atakayokamatwa nayo kuchukuliwa na vijiji vya Milawilila na Mifulu.

15 (1), (6) Kubangua magome ya miti na uchimbaji wa mizizi bila kibali faini yake ni Tshs. 20,000/= na vifaa na mali itataifishwa na kuwa mali ya vijiji vyote viwili.

15 (1), (7) Kuvua samaki katika eneo la msitu bila kibali faini itakuwa ni Tshs. 10,000/= kwa anayevua bila kutumia sumu na Tshs. 30,000/= kwa anayetumia sumu.

15 (1), (8) Kwa mtu yeyote atakayeingia msituni akiwa na shoka, panga, nyengo, msumeno, nyundo faini yake ni Tshs 50,000/= na vifaa vyake vyote alivyokuwa anatumia pamoja na mali kuchukuliwa na vijiji husika.

15 (1), (9) Mgeni mtanzania kuingia katika msitu wa Milawilila bila kibali faini ni Tshs. 30,000/=.

15 (1), (10) Kwa mgeni asiyekuwa mtanzania kama ataingia msituni bila kibali faini yake dola 7 akishindwa kulipa atafikishwa kwenye vyombo vya dola na kufunguliwa mashitaka.

15 (1), (11) Kufanya matambiko msituni kwa ajili ya tiba ya asili (uganga wa kienyeji) bila kibali faini ni kati ya Tshs. 30,000/= na 35,000/=.

15 (1), (12) Kuwinda au kutega wanyama msituni bila kibali faini Tshs 15,000/=.

15 (1), (13) Kuchunga mifugo ndani ya msitu wa Milawilila faini ni Tshs 15,000/=.

15 (1), (14) Kuharibu uoto wa asili msituni kwa kulima au kufyeka faini ni Tshs. 5,000/=;

15 (1), (15) Kutokuwa na kibali kwa shughuli zisizolipiwa ushuru

Faini yake ni Tshs. 5,000/= pamoja na mali kutaifishwa na kijiji.

15 (1), (16) Faini ya kutowajibika kwa viongozi

Faini ni Tshs 5,000/= kwa kila kosa atakalofanya au kuachishwa uongozi.

***Kuwasilisha Kesi***
***Mashauri Mahakamni***

16(1) Iwapo mtu anayetuhumiwa kutenda kosa atakataa kukiri kutenda kosa mbele ya kamati ya mazingira, na mbele ya M/kiti wa kijiji au mbele ya mtendaji wa vijiji, vyombo hivi vya uundaji vitapeleka shauri hilo mahakamani kwa maamuzi zaidi.

16(2) Iwapo mhalifu atashindwa au kukataa kulipa faini , suala hilo litafikishwa mahakamni

16(3) Katika kuendesha kesi mahakamani, itakuwa na haki ya kurejea sheria ndogo za kijiji na wakati mwingine kuamua mhalifu kuadhibiwa kufuatana na sheria hizo. Hii ni pamoja na faini, gharama za usumbufu, fidia za uharibifu, na zilipwe kwa kamati ya mazingira husika.

***Mahakama Kumwamuru Mtuhumiwa Kulipa Faini Kwa Mujibu wa Sheria Na 9 ya Mwaka 1985***

17(1) Katika kuendesha kesi, mahakama itakuwa na haki ya kurejea sheria ndogo za kijiji na wakati mwingine kuamua ikiwa mtuhumiwa amepatikana na kosa kuadhibiwa kufuatana na sheria hizo. Hii ni pamoja na, gharama za usumbufu, fidia kwa kamati za mazingira za vijiji, baada ya mahakama kutoa uamuzi kama ilivyo sehemu ya 170 ya kesi za jinai (Act no.9 ya 1985)

***Sheria ya Msitu Na. 14 ya 2002 Sehemu V (26) Marekebisho***

18 (1) Kama mahakama inataka kutoa hukumu kufuatana na sehemu ya 26 ya sheria za misitu hivyo kamati za mazingira za Mifulu na Milawilila zitakuwa kama mtoa taarifa “Informer” kwa maana ya sehemu ya 99 sheria za misitu cap 14 ya 2002 hizo kamati za misitu za vijiji, aidha Mifulu au Milawilila zitapata nusu ya faini atakayotozwa mhalifu na fedha hizo zitawekwa kwenye akaunti ya **MIFUMILA.**

***Marekebisho Ya Sheria***

19(1) Halmashauri za vijiji vya Mifulu na Milawilila kwa idhini ya mkutano mkuu wa kijiji zinaweza kufanya marekebisho ya sheria hii bila kuharibu au kukiuka madhumuni ya msingi yaliyopelekea kuwepo kwa sheria hii kwa ushauri wa wataalam wa misitu wa kata/tarafa na wilaya.

19(2) Mapendekezo ya mabadiliko yanayopendekezwa kufanywa ni lazima yapelekwe kwa Afisa Misitu wa Wilaya kwa ushauri zaidi.

19(3) Taarifa ya mabadiliko haya ni lazima yatumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Morogoro kupitia afisa maliasili wake.

**Tarehe ya Kuanza**
***Kutumika kwa Sheria Hizi***

20 (1) Sheria hizi ndogo za vijiji zitaanza kutumika rasmi baada ya kupitishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro na baada ya kusainiwa na wenyeviti wa vijiji vya Mifulu na Milawilila.

**Imepitishwa na:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| **1)** | ______________________<br>**Eng. Annah J. Mwahalende**<br>*Mkurugenzi Mtendaji*<br>*Halmashauri (W) Morogoro* | | ________________<br>**Tarehe** |
| **2)** | ______________________<br>**Hamza Mfaume**<br>*Mwenyekiti wa Halmashauri (W) Morogoro* | | ________________<br>**Tarehe** |

**Imetayarishwa na:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| **1)** | ______________________<br>**Omari Rajabu Mdung'u**<br>*Mwenyekiti wa Kijiji cha Mifulu* | | ________________<br>**Tarehe** |
| **2)** | ______________________<br>**Said Ismail Zengwe**<br>*Mwenyekiti wa Kijiji cha Milawilila* | | ________________<br>**Tarehe** |